HOTUBA YA MWENYEKITI WA BARAZA LA TAIFA LA USALAMA BARABARANI MOROGORO TAREHE 26/10/2008

Mgeni Rasmi na Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Mizengo Pinda (MB).,

Makamu Mwenyekiti wa Baraza la Taifa la Usalama Barabarani na Naibu Waziri Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi Mhe. Khamis Kagasheki (Mb).,

Mkuu wa Mkoa wa Morogoro,

Mwakilishi wa Inspekta Jenerali wa Polisi,

Wajumbe wa Baraza la Taifa la Usalama Barabarani,

Wajumbe wa Kamati ya Usalama Barabarani Mkoa wa Morogoro,

Mabibi na Mabwana.

Asalaam Aleikum.

Ndugu Mgeni Rasmi,

Kwa niaba ya Baraza la Taifa la Usalama Barabarani na kwa niaba yangu mimi mwenyewe napenda kuchukua fursa hii kukushukuru kwa kukubali kwako kuwa Mgeni wetu Rasmi katika Maadhimisho ya Wiki ya Nenda kwa Usalama Barabarani.

Kitendo cha kuacha majukumu mengi uliyo nayo na kuamua kuja kushiriki nasi kinaonyesha ni jinsi gani suala la usalama barabarani unavyolipa uzito.

Aidha, napenda kuchukua fursa hii kuwashukuru Wananchi wote wa Mkoa wa Morogoro kupitia kwa Mhe. Mkuu wa Mkoa, kwa kuipokea heshima hii ya kuandaa Maadhimisho haya Kitaifa. Kadhalika tunaishukuru Kamati ya Usalama Barabarani ya Mkoa wa Morogoro kwa kukubali kuwa Mwenyeji wa Maadhimisho haya. Tunawashukuru sana.

Ndugu Mgeni Rasmi,

Baraza la Taifa la Usalama Barabarani liliundwa kwa Sheria ya Usalama Barabarani Na.30 ya mwaka 1973 (Road Traffic Act No.30 of 1973) na kupewa majukumu ya kusimamia shughuli zote za usalama Barabarani. Baraza la Taifa la Usalama Barabarani limekuwa likiandaa Maadhimisho haya ya Wiki ya Nenda kwa Usalama Barabarani tangu 1977 lengo kubwa likiwa ni utoaji wa Elimu ya Usalama Barabarani katika jitihada ya kukabiliana na ajali za barabarani.

Ajali za barabarani bado zinaendelea kutokea na watu wengi kupoteza maisha na majeruhi wengi kubaki na ulemavu wa maisha. Baraza la Taifa la Usalama Barabarani kwa kushirikiana na Jeshi la Polisi Tumekuwa tunaelimisha na kukemea Wamiliki na Madereva wasiopenda kutii Sheria za Usalama Barabarani, tukiwataka kufuata Sheria za Usalama Barabarani. Lazima tukiri, hali bado hairidhishi.

Ndugu Mgeni Rasmi,

Ajali za barabarani zimekuwa zikisababishwa na mambo makuu matatu:

- Makosa ya Kibinadamu (Human Error).
- Ubovu wa Magari (Deffective Vehicles),
- Mazingira ya barabara (Environmental Factors).

Kati ya sababu zote tatu, makosa ya Kibinaadamu yanachangia takriban asilimia 78 ya ajali zote za barabarani zinazotokea nchini.

Makosa haya ni pamoja na:

- Kuendesha gari kwa Mwendokasi
- Dereva kuendesha gari akiwa amelewa
- Kuzidisha Mizigo au Abiria

Ubovu wa magari pia huchangia kwa kiasi kikubwa ajali za barabarani.

Aidha, hali ya barabara zetu pia huchangia ongezeko la ajali za barabarani. Barabara zetu nyingi ni nyembamba kwa magari makubwa kupishana. Baadhi ya barabara hazina alama za barabara za kuongoza watumiaji wa barabara. Tunatambua jitihada za Serikali katika kukarabati na kujenga barabara mpya, lakini upo umuhimu mkubwa wa Serikali

zetu za mitaa kulipa uzito eneo hili hasa katika kuukabili uharibifu wa barabara mara tu unapoanza kutokea.

Baraza la Taifa la Usalama Barabarani kupitia Kikosi cha Usalama Barabarani limekuwa likichukua hatua za kukabiliana na hali hiyo kama ifuatavyo:

- Kufanya Highway Patrol kwa lengo la kudhibiti mabasi yaendayo kasi
- Kufanya ukaguzi wa Leseni ili kubaini kama Madereva wote wana leseni halali kulingana na gari analoendesha
- Utoaji wa Elimu ya Usalama Barabarani kwa njia ya Redio, Televisheni, Vipeperushi na Magazeti
- Kupitia Maadhimisho haya tunatoa fursa kwa Wananchi wote kuja kupata Elimu ya Usalama Barabarani
- Kushirikisha Wadau wengi wa Usalama Barabarani katika suala zima la usalama barabarani.
- Kuanzisha maeneo yaliyokithiri kwa ajali na kushirikiana na Wadau wengine e.g. TANROADS kwa lengo la kudhibiti maeneo hayo.

Ndugu Mgeni Rasmi,

Pamoja na juhudi hizi zinazofanywa na Baraza la Taifa la Usalama Barabarani, bado kuna changamoto mbalimbali ambazo tunadhani zikitekelezwa, Baraza litafanya kazi zake kwa ufanisi zaidi. Changamoto hizo ni pamoja na zifuatazo:

1. Baraza hili tangu kuundwa kwake, tofauti na Mabaraza mengine halipewi ruzuku, kwa hiyo Baraza limekuwa likitekeleza majukumu yake kwa misaada kutoka kwa Wadau mbalimbali wa Usalama Barabarani.

   Tunaomba Serikali ilipatie ruzuku Baraza hili, liweze kutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa sheria.

2. Tunaomba Serikali kupiga marufuku magari ambayo yamekwishatumika zaidi ya miaka mitano yasiruhusiwe kuingia hapa nchini, kwa sababu kwa kuingia kwa magari haya kumekuwa ni chanzo cha magari mabovu nchini kuongezeka.

3. Kiwango cha Faini kiongezwe; kwa sasa kosa moja la Usalama Barabarani kwa mujibu wa Sheria ya Usalama Barabarani (The Road Traffic Act.1973) Notification Traffic Offences iliyopangwa kwenye Tangazo la Serikali Govt. Notice No.249 – 30/06/2000 ni Shs.20,000/=. Tunaomba faini hizi ziongezwe iwe kubwa na ambayo itawalazimisha Madereva wa magari kutii Sheria za Usalama Barabarani.

4. Serikali ipunguze ushuru wa mabasi ili watu wanunue mabasi mapya kuondokana na haya yaliyotumika (Mitumba).

Ndugu Mgeni Rasmi,

Baada ya kusema hayo machache, napenda kurudia kukushukuru wewe binafsi na Serikali kwa ujumla kwa kuendelea kushirikiana na Baraza la Taifa la Usalama Barabarani katika jitihada zake za kuhakikisha Usalama Barabarani unaimarika.

Aidha, naishukuru pia Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa misaada na miongozo yao ambayo wamekuwa wakitupatia katika kuongoza Baraza hili, niwashukuru Wizara ya Miundombinu na Makampuni yote yaliyotufadhili kwa njia moja au nyingine kufanikisha Maadhimisho haya.

Mhe. Waziri Mkuu,

Naomba sasa nikukaribishe, utufanyie mambo matatu:
Kwanza, utoe zawadi na vyeti vya kutambua mchango wa kila aliyetusaidia kwenye jukumu letu. Pili, utuzindulie Kanuni za Barabarani, na mwisho utuhutubie.

"AJALI ZA BARABARANI ZINAEPUKIKA, CHUKUA TAHADHARI"

KARIBU SANA